



Zimeteremshwa kwangu aya, hazijawahi kuonekana mfano wake katu, sura mbili za kinga

Imepokelewa kutoka kwa Uqba bin Aamir -radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake- amesema: Amesema Mtume rehema na amani ziwe juu yake: "Zimeteremshwa kwangu aya, hazijawahi kuonekana mfano wake katu, sura mbili za kinga"

[Sahihi] [Imepokelewa na Imamu Muslim]

Ameleza Uqba bin Aamir radhi za Allah ziwe juu yake yakwamba Mtume rehema na amani ziwe juu yake alisema kumwambia: Usiku huu Mwenyezi Mungu kaniteremshia aya, hazijawahi kuonekana mfano wake katu -yaani katika kuomba kinga- nazo ni sura mbili za kinga: Suratu (Qul Auudhubirabbil falaq), na suratu (Qul Auudhubirabbinnas).

<https://sunnah.global/hadeeth/sw/show/65448>

النجاة الخيرية
ALNAJAT CHARITY

